

## HALMASHAURI YA WILAYA-NGARA

### UTEKELEZAJI WA HUDUMA ZA KIFUA KIKUU

#### Utangulizi

Wilaya ya Ngara ni miongoni mwa wilaya 8 katika mkoa wa Kagera. Inao wakazi wapatao 359,164 kulingana na sensa ya 2012. Inavyo vituo 61 vya kutolea huduma za afya; Hospitali 3, Vituo vya Afya 5 na Zahanati 53.

Katika vituo hivyo 61, vituo 10 tu hutoa huduma za ugunduzi na matibabu ya Kifua Kikuu (Hospitali 3 za Murgwanza, Rulenge na Nyamiaga, Vituo vya Afya 4 vya Mabawe, Murusagamba, Bukiriro na Lukole pamoja na Zahanati 2 za Kabanga Gov, Buhororo na Lourdes).

Ugonjwa wa Kifua Kikuu umeendelea kuwa tishio na unaongezeka kwa kasi kutokana na kuwa na jamii yenye maabukizi ya VVU/UKIMWI. Kwa sasa inakadiriwa kuwa, kati ya watu 100,000 kuna watu wapatao 528 wenye maambukizi ya Kifua Kikuu. Wizara inaagiza zifanyike jitihada mbalimbali kuwatafuta watu hawa walio ndani ya jamii, ili kuzuia athari za Kifua Kikuu katika jamii.

Halmashauri ya wilaya ya Ngara, Idara ya Afya imeendelea kutekeleza mikakati ya kupambana na Ugonjwa wa Kifua Kikuu kama Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, jinsia, wazee na watoto inavyoelekeza kupitia sera mbalimbali.

Jedwali lifuatalo linaonesha ugunduzi wa wagonjwa kwa mwaka 2016, 2017 na 2018.

	<b>Waliogundulika</b>	<b>Waliopima VVU</b>	<b>Waliokutwa na maambukizi ya VVU</b>
<b>2016</b>	170	170	48
<b>2017</b>	183	183	46
<b>2018(Jan-Jun)</b>	84	84	14

#### Mafanikio

- Kuwepo kwa dawa za kutibu ugonjwa wa Kifua Kikuu katika vituo vya tiba, idara imejitahidi kuwezesha uwepo wa dawa muda wote, hivyo wagonjwa kutokatisha dozi zao.
- Kuongeza uibuaji wa wagonjwa kwa asilimia 8 kutoka 2016 hadi 2017

#### Changamoto

- Uwepo wa vituo vichache vinavyofanya ugunduzi; Kulingana na hali ya kijiografia ya wilaya yetu vituo 10 tulivyo navyo ni vichache na mbaya zaidi nusu vipo mjini hivyo wananchi wengi walio vijijini kukosa huduma ya upimaji.
- Ukosefu wa miundo mbinu na wataalamu;

- Licha ya uwepo wa vituo hivyo 10, ni vituo 3 tu vyenye huduma za uhakika za upimaji y.n hospitali tatu. Vituo vilivyobaki vina upungufu wa miundombinu ya maabara inayokubalika na vingine kutokuwa na wataalamu wanaoagizwa kisera.
  - Vituo vingi vya kutolea huduma za Afya kutokuwa na miundombinu ya maabara hivyo kushindwa kuongeza vituo vya uguduzi kwa minajili ya kusogeza huduma hiyo karibu kwa wananchi.
  - Uhaba wa wataalamu wa maabara na matabibu wilayani, vituo vingi vinaendeshwa na wauguzi.
- Watumishi vituoni kuwa na uelewa mdogo juu ya Kifua Kikuu.
  - Kufa kwa vikundi vya Ex-TBs vilivyokuwa vinasaidia uibuaji wa wagonjwa; Makundi haya yalikuwa kutokana na kukosa uwezeshaji kifedha, Mfuko wa dunia, GF ulikuwa unafadhili vikundi hivi ila kwa kipindi kirefu vimekosa ufadhili.

Changamoto hizo hapo juu zimepelekea wilaya kutofikia malengo ya uibuaji wa wagonjwa wa Kifua Kikuu.

### **Mikakati**

Ili kuibua wagonjwa wengi Zaidi katika jitihada za kufikia lengo la wizara la kugundua wagonjwa 528 kwa mwaka (wastani wa wagonjwa 132 kwa robo) ifikapo 2020, idara inakusudia kutekeleza mikakati ifuatayo.

- Kuongeza vituo vya kufanya ugunduzi;
  - Idara inakusudia kufanya maongezi na vituo vya watu binafsi ili wasaidie kutoa huduma hii kwani haina gharama. Vituo hivyo ni Zahanati ya Huduma, Zahanati ya Amen na Zahanati ya Kabanga Private.
  - Vilevile kufufua/kuhuisha vituo vilivyokuwa vikitoa huduma hapo mwanzo ili vianze upya, Kituo cha Afya Tumaini. Hivyo tunatarajia ifikapo Desemba, 2018 vituo hivi vitakuwa vimeishaanza kufanya kazi na kufanya idadi ya vituo vinavyofanya ugunduzi kuwa 14.
- Kuimarisha utendaji kazi wa wahudumu wa afya majumbani ambao wamepatiwa mafunzo ya Kifua Kikuu kwenye jamii na wahisani/wadau AMREF ili kuweza kutekeleza mikakati wa *index case finding*.
- Kuimarisha ziara za usimamizi shirikishi na tegemezo vituoni ili kuamsha uelewa wa watumishi juu ya ugonjwa wa Kifua Kikuu.
- Kufanya uhakiki katika maabara za vituo vinavyofanya ugunduzi ili kuhakikisha matokeo yaliyo bora ya vipimo vinavyofanyika.
- Kutoa elimu ya Afya kwa njia ya redio-Redio Kwizera na kutembelea mashule na magereza kutoa elimu ya Afya.

Wilaya inaishukuru serikali kupitia mpango wa kupambana na kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma kwa kupatiwa mashine ya Gene Xpart ili kusaidia uibuaji wa wagonjwa wa Kifua Kikuu Sugu ambacho kimeanza kushamiri kwenye jamii. Kupatiwa mashine hii ya Gene X-part kumetatua changamoto iliyokuwepo ya usafirishaji wa sampuli kwenda mkoani.